# Vyeti, nyaraka 'feki' ni

NA BETTY KANGONGA

IDADI kubwa ya nyaraka zinazotumika kusaka ajira vikiwemo vyeti vya elimu ya sekondari, vyuo vikuu vya ndani na nje, vyeti vya ndoa, stika za bima za magari na bodaboda na nyaraka kutoka Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), zimebainika kuwa ni feki.

Hali hiyo imebainishwa jana na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Casian Chibogoyo, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

Chibogoyo alitaja nyaraka nyingine feki zilizokamatwa wiki hii katika operesheni maalumu na maofisa wa ofisi yake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ni mihuri ya mabalozi mbalimbali nchini, kadi za magari, stakabadhi za malipo ya serikali na utambulisho wa ukaazi kwa watu wasio raia.

Chibogoyo alisema katika operesheni hiyo iliyoongozwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, walibaini kuzagaa kwa nyaraka hizo feki, vikiwemo vyeti vya kitaaluma kutoka Chuo Kikuu cha Kampala na cheti cha ndoa cha Kanisa Katoliki la Mtakatifu Maria Magomeni.

Mpiga chapa huyo aliutaka uongozi wa Jiji la Tanga kuwa makini na stika za magari baada ya kubaini kuwa maboksi matatu ya stika hizo, zilizokamatwa, zilikuwa katika hatua za mwisho kutaka kusafirishwa kwenda mkoani Tanga, hivyo kuna uwezekano wa kuwapo maboksi mengine kufikishwa mkoani humo.

"Tumejipanga kupambana na uhalifu huo ambao ni zaidi ya ujambazi, maana watu hao wana lengo la kuwaua Watanzania kwa vyeti vya kughushi vikiwemo vya kidaktari," alisema.

Chibogoyo aliwaomba waajiri nchini kuanza mchakato wa kuhakiki vyeti vya watumishi wao na kuwasiliana na ofisi yake ili kubaini vilivyoghushiwa.

Aliutaka uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha unafanya ukaguzi kwani nyaraka nyingi zilizokamatwa ni za malipo kutoka TRA.

Alisema kuwa vituo vinavyofanya ujambazi huo vinajulikana, akitolea mfano wa kuwepo kwa mama lishe mmoja katika eneo la katikati ya jiji ambaye amekuwa akiuza stika hizo za magari zilizohifadhiwa kwenye friji bovu.

"Huyo mama lishe, anauza vyakula, lakini pembeni yake kuna friji bovu limesheheni stika. Ukifika hapo huwezi kujua kama ana biashara ya stika, kumbe ndiye mwenyewe," alisema Chibogoyo na kuongeza kuwa mama huyo yumo kwenye mikono salama.

Chibogoyo alisema ni hatari kuona vyeti vya kughushi vikimilikiwa na raia wa kigeni ambao hawajaratibiwa, hivyo usalama wa nchi umo shakani.

Alisema upatikanaji wa nyaraka hizo feki, unaweza kuvuruga mipango ya nchi na kuiweka katika hali isiyo salama na hata kuleta mifarakano katika jamii.

"Tatizo la vyeti vya kughushi ni kubwa, ni wakati sasa wa kushirikiana kwa idara zote ili kuweza kutokomeza janga hili ambalo linazidi kutisha," alisema.

Alisema kuwa operesheni hiyo ilibaini kuwapo vibali feki vya pikipiki na magari hivyo kuna uwezekano mkubwa bodaboda nyingi zina stika feki, hivyo kuikosesha serikali mapato.

Chibogoyo alitoa onyo kuwa kuanzia sasa mitambo itakayonaswa kuchapisha nyaraka feki itataifishwa na wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema kughushi nyaraka ni kosa la jinai na adhabu yake ni kutupwa jela miaka 20.

"Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 Na. 3, ibara ya sita inakataza kuwa na nyaraka, mihuri, karatasi maalumu na kumiliki taarifa za serikali isivyo halali na kosa lake ni adhabu ya miaka 20," alisema.

Alisema sheria ya udhibiti wa vielelezo vya taifa, nembo na bendera, hairuhusiwi kuvitumia kibiashara wala


Climate Strategies

3rd GLOBAL CLIMATE POLICY CONFERENC

IMPLEMENTING THE PARIS AGREEMENT

NEW RESEARCH SOLUTIONS FOR DEVELOPING COUNTRIES

13th - 14th July 2016, DAR ES SALAAM.

The Stanley Foundation



itute

# Vyeti, nyaraka 'feki' ni janga

NA BETTY KANGONGA

IDADI kubwa ya nyaraka zinazotumika kusaka ajira vikiwemo vyeti vya elimu ya sekondari, vyuo vikuu vya ndani na nje, vyeti vya ndoa, stika za bima za magari na bodaboda na nyaraka kutoka Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), zimebainika kuwa ni feki.

Hali hiyo imebainishwa jana na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Casian Chibogoyo, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

Chibogoyo alitaja nyaraka nyingine feki zilizokamatwa wiki hii katika operesheni maalumu na maofisa wa ofisi yake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ni mihuri ya mabalozi mbalimbali nchini, kadi za magari, stakabadhi za malipo ya serikali na utambulisho wa ukaazi kwa watu wasio raia.

Chibogoyo alisema katika operesheni hiyo iliyoongozwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, walibaini kuzagaa kwa nyaraka hizo feki, vikiwemo vyeti vya kitaaluma kutoka Chuo Kikuu cha Kampala na cheti cha ndoa cha Kanisa Katoliki la Mtakatifu Maria Magomeni.

Mpiga chapa huyo aliutaka uongozi wa Jiji la Tanga kuwa makini na stika za magari baada ya kubaini kuwa maboksi matatu ya stika hizo, zilizokamatwa, zilikuwa katika hatua za mwisho kutaka kusafirishwa kwenda mkoani Tanga, hivyo kuna uwezekano wa kuwapo maboksi mengine kufikishwa mkoani humo.

"Tumejipanga kupambana na uhalifu huo ambao ni zaidi ya ujambazi, maana watu hao wana lengo la kuwaua Watanzania kwa vyeti vya kughushi vikiwemo vya kidaktari," alisema.

Chibogoyo aliwaomba waajiri nchini kuanza mchakato wa kuhakiki vyeti vya watumishi wao na kuwasiliana na ofisi yake ili kubaini vilivyoghushiwa.

Aliutaka uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha unafanya ukaguzi kwani nyaraka nyingi zilizokamatwa ni za malipo kutoka TRA.

Alisema kuwa vituo vinavyofanya ujambazi huo vinajulikana, akitolea mfano wa kuwepo kwa mama lishe mmoja katika eneo la katikati ya jiji ambaye amekuwa akiuza stika hizo za magari zilizohifadhiwa kwenye friji bovu.

"Huyo mama lishe, anauza vyakula, lakini pembeni yake kuna friji bovu limesheheni stika. Ukifika hapo huwezi kujua kama ana biashara ya stika, kumbe ndiye mwenyewe," alisema Chibogoyo na kuongeza kuwa mama huyo yumo kwenye mikono salama.

Chibogoyo alisema ni hatari kuona vyeti vya kughushi vikimilikiwa na raia wa kigeni ambao hawajaratibiwa, hivyo usalama wa nchi umo shakani.

Alisema upatikanaji wa nyaraka hizo feki, unaweza kuvuruga mipango ya nchi na kuiweka katika hali isiyo salama na hata kuleta mifarakano katika jamii.

"Tatizo la vyeti vya kughushi ni kubwa, ni wakati sasa wa kushirikiana kwa idara zote ili kuweza kutokomeza janga hili ambalo linazidi kutisha," alisema.

Alisema kuwa operesheni hiyo ilibaini kuwapo vibali feki vya pikipiki na magari hivyo kuna uwezekano mkubwa bodaboda nyingi zina stika feki, hivyo kuikosesha serikali mapato.

Chibogoyo alitoa onyo kuwa kuanzia sasa mitambo itakayonaswa kuchapisha nyaraka feki itataifishwa na wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema kughushi nyaraka ni kosa la jinai na adhabu yake ni kutupwa jela miaka 20.

"Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 Na. 3, ibara ya sita inakataza kuwa na nyaraka, mihuri, karatasi maalumu na kumiliki taarifa za serikali isivyo halali na kosa lake ni adhabu ya miaka 20," alisema.


Alisema sheria ya udhibiti wa vielelezo vya taifa, nembo na bendera, hairuhusiwi kuvitumia kibiashara wala kufanya 'modification'.

"Watakaokamatwa wakijihusisha na utengenezaji wa nyaraka bandia na mitambo yao itataifishwa kama ilivyoelezwa pia kwenye Sheria ya Makosa ya Jinai," alisema.

Mwanzoni mwa wiki hii, Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Simon Sirro, aliwakamata watu watatu wanaodaiwa kuwa vinara wa kutengeneza vyeti bandia na nyaraka mbalimbali za serikali.

Desemba 19, mwaka jana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Angella Kairuki, alibaini kuwa watumishi 219 miongoni mwa 704 wa serikali wameajiriwa kwa kutumia vyeti vya kughushi.

Kutokana na sakata hilo, Kairuki aliagiza Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu (Utumishi), kuwachukulia hatua watumishi hao waliotumia vyeti hivyo kupata ajira serikalini.




*Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akifungua Mkutano wa Tatu wa Sera za Mabadiliko ya Tabia Nchi jijini Dar es Salaam juzi ulioandaliwa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Climate Strategies. Mkutano huo ulijumuisha watafiti na watunga sera 80 kutoka nchi zaidi ya 10 nje na ndani ya Afrika chini ya kaulimbiu 'Kutekeleza Makubaliano ya Paris - Suluhu Mpya za Utafiti kwa nchi zinazoendelea'. Kutoka kulia ni Mwenyekiti wa mkutano huo, Chuks Okereke, Waziri wa Nchi, Mazingira na Muungano, January Makamba na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Prof. Joseph Semboja. (Na Mpiga Picha Wetu).*